Shukurani ya Paulo – Unakumbuka

na

Ellis Forsman

Shukurani ya Paulo – Unakumbuka

na

Ellis Forsman

Oktoba 14, 2011

Shukurani ya Paulo – Unakumbuka

Fil. 4:10-23

Katika kifungu cha mwisho wa kitabu cha Wafilipi, Paulo anataja nyakati ambazo zilishinikiza kuandika waraka huu.

Katika mistari hii tunapata shukurani za Paulo zimeonyeshwa, "Asanteni – Unakumbuka", kama hamtajali.

Fil. 4:10-23, "*Nalifurahi sana katika Bwana, kwa kuwa sasa mwisho mmehuisha tena fikira zenu kwa ajili yangu, kama vile mlivyokuwa mkinifikiri hali yangu; lakini hamkupata nafasi. Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote; na katika mambo yo yote nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. Lakini mlifanya vema mliposhiriki nami katika dhiki yangu. Nanyi pia ninyi wenyewe mnajua enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lo lote lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi pekee yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja. Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu. Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu. Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu. Sasa atukuzwe Mungu, Baba yetu, milele na milele. Amina. Mnisalimie kila mtakatifu katika Kristo Yesu. Ndugu walio pamoja nami wawasalimu. Watakatifu wote wawasalimu, hasa wao walio wa nyumbani mwa Kaisari. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zetu.*

Katika misitari hii ya mwisho, kuna baadhi ya vitu vya kukumbuka na ningependa kuzisisitiza:

- Ukarimu wa Wafilipi
- Kutosheka kwa Paulo
- Nguvu ya Kristo
- Utajiri wa Mungu
- Salamu za watakatifu

Ukarimu wa Wafilipi

Kama inavyoelezwa na Paulo.

Zingatia hasa misitari ya 10, 14-18:

- Fil. 4:10, "*Nalifurahi sana katika Bwana kwa kuwa sasa mwisho mmehuisha tena fikira zenu kwa ajili yangu, kama vile mlivyokuwa mkinifikiri hali yangu; lakini hamkupata nafasi.*"
- Fil. 4:14-18, "*Lakini mlifanya vema mliposhiriki nami katika dhiki yangu. Nanyi pia ninyi wenyewe mnajua enyi Wafilipi ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi pekee yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mlinileta msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja. Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu. Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu.*"

Wazi wazi, walionyesha "mwendelezo" wa msaada na kumjali mtume.

Mara ya kwanza Paulo alipotoka Makedonia, walishiriki pamoja naye. Hata kabla ya kuondoka Makedonia, alipokuwa angali Thesalonike, walituma msaada mara nyingi.

Sasa mwishoni, alipokuwa gerezani (kushikwa ndani ya nyumba) huko Rumi, walituma zawadi kwa mkono wa Epafrodito.

Ni picha nzuri kiasi gani ya ushirika kati ya kusanyiko na mwinjilisti!

Kuna wachache sana leo ambao hawamsaidii Ndg. Otto Alvarez wakisema kwamba wanadhani ni tapeli, kwamba anaweka mfukoni pesa ambazo makusanyiko yanamtumia. Hawana uthibitisho, isipokuwa uoga. Ni jinsi gani hawafanani ukilinganisha na kanisa la Filipi na tabia zao dhidi ya Ndg. Paulo katika kazi yake ya uinjilisti.

Kitu kingine cha kuzingatia katika kifungu hiki ni…

Kutosheka Kwa Paulo

Kama ilivyoelezwa na Paulo.

Maelezo yake ya shukurani haikuonyesha kwamba alikuwa katika hitaji kuu.

Fil. 4:11, "*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji…*"

Maana Paulo alitosheka sana na "hali" aliyojikuta akiwemo. Fil. 4:11, "*…maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo.*"

"Kuridhika" huku ni kitu ambacho alijifunza. Fil. 4:11-12, "*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote na katika mambo yo yote nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa.*"

"Ufunguo" wa kutosheka kwa Paulo ulikuwa ni nini?

Kama ilivyoelezwa katika Fil. 4:13, inajumuisha nguvu alizopewa na Bwana. Fil. 4:13, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*"

- Kristo alimuwezesha kuridhika iwe ameshiba au njaa.
- Kristo alimuwezesha kuridhika iwe anavyo vingi au anahitaji.

Sehemu ya nguvu hii kutoka kwa Bwana ingeweza kuwa mtazamo halisi ambao yawezekana Paulo alipokea kwa Bwana.

Mtazamo halisi dhidi ya kifo na uzima. Fil. 1:21-24, "*Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo na kufa ni faida. Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi nitakalolichagua silitambui. Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo; maana ni vizuri zaidi sana; bali kudumu katika mwili kwahitajiwa zaidi kwa ajili yenu.*"

Mtazamo halisi kuhusu umuhimu wa kweli katika maisha.

1 Tim. 6:6-8, "*Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo.*"

Baada ya kueleza nguvu alizopewa na Bwana, hebu tuangalie kidogo kwa ukaribu kuhusu…

Nguvu ya Kristo

Hakika kuna nguvu ipatikanayo kwa Wakristo!

Kama Paulo anavyoonyesha, nguvu hii inamuwezesha mtu kufanya vitu vyote ambavyo ni vya muhimu katika kumtumikia Bwana. Fil. 4:13, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*"

Tunajifunza zaidi kuhusu nguvu hii ya ajabu katika waraka wa Paulo kwa Waefeso.

Ni nguvu ambayo Paulo alitaka wao wafahamu

Efe. 1:18-19, "*Macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi katika watakatifu*

jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu ***tuaminio*** *jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake."*

Ni nguvu inayofanana na ile iliyotumiwa kwa kumfufua Yesu kutoka katika wafu, na ikamweka katika mkono wa kuume wa Mungu!

Efe. 1:19-21, "*Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu; akamweka katika mkono wake wa kuume katika ulimwengu war oho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia;*"

Paulo aliona nguvu kama hiyo kwa Roho Mtakatifu, akikaa ndani ya Wakristo.

Rum. 8:11-14, "*Lakini ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu. Basi kama ni hivyo, ndugu, tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho mtaishi. Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.*"

Aliomba kwamba Mungu aweze kuwatia nguvu Waefeso na nguvu kama hiyo, ambayo ingewawezesha kufanya mambo makuu.

- Efe. 3:16, "*Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanyia imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake, katika utu wa ndani.*"
- Efe. 3:20-21, "*Basi atukuzwe yeye awzaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.*"

Kwa maneno mengine, Roho kama chombo, Mungu na Kristo wanawawezesha Wakristo kufanya yote wanayohitajika kufanyika!

Faida ya nguvu hii.

Hatuko peke yetu katika juhudi za "kutimiza wokovu wetu wenyewe".

Fil. 2:12-13, "*Basi wapendwa wangu kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.*"

Hakuna udhuru ya kutofanya ambacho Mungu anapenda!

Tunapoanguka , mara nyingi inakuwa ni tatizo la matakwa, sio uwezo! (vile vile na wale walioko nje ya Kristo, ilipo tatizo la uwezo).

Rum. 7:22-25, "*Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka na ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.*"

Kwa Wakristo wanaotenda dhambi kwa kupenda, sio kwamba hawawezi kufanya mapenzi ya Mungu, isipokuwa hawataki!

Lakini kwa sababu wakati mwingine tunafanya dhambi kwa kukiuka mara nyingi tuko katika hitaji la damu ya Yesu inayosafisha.

Tunapofahamu mapenzi ya Mungu, hakuna udhuru ya kutokuifanya!

Ni baraka ya ajabu kiasi gani kwa wale walio ndani ya Kristo, kuwa na uwezo huo! Lakini bado kuna elezo za baraka zaidi katika fungu letu la maandiko, kama tunavyoona kinachosemwa kuhusu…

Utajiri wa Mungu

Kama inavyofafanuliwa na Paulo.

Haya ni "utajiri wa utukufu" ambazo Mungu anatoa kupitia Yesu Kristo.

Fil. 4:19, ""*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.*"

Lazima mtu awe "ndani ya Kristo" ili aweze kufurahia "utajiri huu".

Hakika, "ndani ya Kristo" ndiyo sehemu ambapo Mungu anatoa kila baraka za rohoni.

Efe. 1:3-13, "*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho* ***ndani yake Kristo****; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe*

kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. Katika yeye huyo kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi sawasawa na wingi wa neema yake. Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi; akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake sawasawa na uradhi wake, aliokusudia katika yeye huyo. Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote ***katika Kristo****, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam,* ***katika yeye huyo****; na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliotangulia kumwekea* ***Kristo tumaini letu****. Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.*"

Kumbuka matumizi ya neno "ndani yake Kristo" au "katika yeye".

Si kwamba Mungu anatupatia mahitaji ya kiroho pekee, bali "mahitaji yako yote"; ambayo inajumuisha umuhimu wa maisha, kama chakula na mavazi.

Kama Yesu mwenyewe alivyofundisha.

Mat. 6:30-33, "*Basi ikiwa Mungu huyavisha hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba.? Msisumbuke basi mkisema, tule nini? au tunywe nini?au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa* ***mnahitaji*** *hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Pamoja na "utajiri" kama huuu, kwa nini tusitosheke?

Tuna wingi wa baraka za "kiroho" na uhakika wa mahitaji yale ya "kimwili" tunawezaje kupungukiwa tusiporidhika?

Mungu na atusamehe tunapochukua "utajiri" huu kirahisi na kuanza kujisikia kuwa hatutosheki na kile tulicho nacho!

Mwisho, tunakumbuka…

Salamu za Watakatifu

Kama tulivyosoma hapa katika Wafilipi…

Kwanza Paulo anatuma salamu zake. Fil. 4:21, "*Mnisalimie kila mtakatifu katika Kristo Yesu…*"

Ndugu waliokuwa pamoja naye (wale waliomtembelea alipokuwa katika kifungo cha nyumbani) pia walituma salamu zao. Fil. 4:21, "*…ndugu walio pamoja nami wawasalimu.*"

Alafu "watakatifu wote" wakatuma salamu zao (Wakristo wote waliokuwa katika Rumi). Fil. 4:22, "*Watakatifu wote wawasalimu hasa wao walio wa nyumbani mwa Kaisari.*"

Tendo rahisi ya salamu inaweza kutumika katika sehemu muhimu.

Waziwazi Paulo alifikiria hivyo.

- Rum. 16:3-16, "*Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu; waliokuwa tayari hata kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu; ambao ninawashukuru wala si mimi tu, ila na makanisa ya mataifa pia; nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao. Nisalimieni Epainero, mpenzi wangu, aliye malimbuko ya Asia kwa Kristo. Nisalimieni Mariamu, aliyejitaabisha sana kwa ajili yenu. Nisalimieni Androniko na Yunia, jamaa zangu waliofungwa pamoja nami, ambao ni maarufu miongoni mwa mitume; nao walikuwa katika Kristo kabla yangu. Nisalimieni Ampliato, mpenzi wangu katika Bwana. Nisalimieni Urbano mtenda kazi pamoja nami katika Kristo, na Stakisi, mpenzi wangu. Nisalimieni Apele mwenye kukubaliwa katika Kristo. Nisalimieni watu wa nyumbani mwa Aristobulo. Nisalimieni Herodioni, jamaa yangu. Nisalimieni watu wa nyumbani mwa Narkiso, walio katika Bwana. Nisalimieni Trifaina na Trifosa, wenye bidii katika Bwana, nisalimieni Persisi, mpenzi aliyejitahidi sana katika Bwana. Nisalimieni Rufo, mteule katika Bwana, na mamaye aliye mama yangu pia. Nisalimieni Asinkrito, Flegoni, Herme, Patroba, Herma na ndugu walio pamoja nao. Nisalimieni Filologo na Yulia, Nerea na dada yake, na Olimpa, na watakatifu wote walio pamoja nao. Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*"

- Rum. 16:21-23, "*Timotheo mtendakazi pamoja nami, awasalimu, na Lukio na Yasoni, na Sosipatro, jamaa zangu. Mimi Tertio, niliyeandika waraka huu, nawasalimu katika Bwana. Gayo mwenyeji wangu na wa kanisa lote pia awasalimu. Erasto, wakili wa mji awasalimu, na Kwarto, ndugu yetu.*"

Baadhi ya faida zinazowezekana kwa kusalimiana.

- Kusalimiana kunaonyesha upendo wetu na shukurani kwa kila mmoja.

- Kusalimiana kila mara (kwa barua au ana kwa ana) huboresha uhusiano tulionao kama ndugu katika Kristo.

Kumbuka kwamba Paulo alipenda kusalimia "kila" mtakatifu katika Kristo Yesu; hakuna nafasi ya upendeleo hapa! Fil. 4:21, "*Mnisalimie kila mtakatifu aliye katika Kristo Yesu. Ndugu walio pamoja nami wawasalimu.*"

Jinsi tunavyosalimu (au tunashindwa kusalimu) Wakristo wengine katika makusanyiko yetu hufunua mengi juu yetu wenyewe.

Tunapowasalimu inaonyesha kwamba tunawajali na kuwapenda pasipo upendeleo.

Hitimisho

Haya ni baadhi ya vitu tunavyoweza kuwa navyo katika "shukuru-unakumbuka".

- Ukarimu wa Wafilipi
- Kutosheka kwa Paulo
- Nguvu ya Kristo
- Utajiri wa Mungu
- Salamu za watakatifu

Ambacho hiki hufunua ni ubora wa juu wa uzima ulioonjwa na wale walio katika Kristo!

Ambao bila kujali magumu alioyapitia Paulo bado angeweza kuhisi na kuandika barua hii kama waraka kwa Wafilipi!

Tunapofunga somo hili katika waraka huu wa ajabu, ninawaachia maneno mawili: "utukufu" na "neema".

- Fil. 4:20, "*Sasa atukuzwe Mungu, Baba yetu, milele na milele. Amina.*"
- Fil. 4:23, "*Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu.*"

Je umepokea neema ya ajabu ya Bwana wetu katika maisha yako, kwa kutii injili yake? Je unaishi kwa kutoa utukufu kwa Mungu, katika kunena na matendo?

Sehemu hii ya neno la Mungu kama waraka kwa Wafilipi ikuvuvie kufanya yote!